# KICHAA CHA MBWA (RABIES)

Na Augustino Chengula

## UTANGULIZI

Kichaa cha mbwa ni ugonjwa hatari sana unaowapata **wanyama wote wanyonyeshao** akiwemo mwanadamu na unapatikana nchi zote duniani isipokuwa katika bara la Antarctica. Kuna nchi ambazo zimefanikiwa kuuondoa ugonjwa huu kulingana na njia bora walizoweka na kuzitii za kupambana na ugonjwa huu. Lakini kuna baadhi ya nchi hasa zinazoendelea (ikiwemo Tanzania) ugonjwa huu umendelea kujitokeza na kusababisha vifo kwa watu wake. Takwimu zinaonyesha kuwa watu kati 50,000 hadi 70,000 hufa kila mwaka duniani kote, hii si namba ndogo hasa tunapozunguzia uhai wa binadamu unaopaswa kulindwa kwa njia zote.

Historia inaonyesha kuwa ugonjwa huu umekuwepo tangu miaka ya 2300 kabla ya kuja kwa Kristo duniani na kwa mara ya kwanza wasemekana kutokea kati ya Afrika na Asia. Kutokea hapo ugonjwa ukaanza kusambaa dunia nzima na ukaendelea kuisumbua dunia sana. Uvumbuzi wa chanjo uliofanywa na mwana sayansi marehemu Louis Pasteur mwaka 1885 ukaleta matumaini makubwa sana kwa tatizo hili japo haukuweza kulimaliza.



Watu wa kale walivyokuwa wakimshughulikia mbwa mwenye kichaa

Ugonjwa huu unasababishwa na kiitwacho ***kirusi cha rabies*** (rabies virus) katika familia ya **Rhabdovirus**. Virusi hawa wanashambulia mfumo wa fahamu na mara zote hupita mfumo wa fahamu hadi kwenye mfumo kati wa fahamu toka pale kinapoingilia kwenye mwili wa mnyama.



Picha ya virusi wa kichaa cha mbwa wenye umbo la monowari

**WANYAMA WANAOWEZA KUPATA KICHAA CHA MBWA**

Wanyama wote wanaonyonyesha wanaojulikana kisayansi kwa jina la mamalia wanauwezo wa kupata ugonjwa huu. Mfano wa wanyama hao ni kama mwanadamu, mbwa, paka, ng'ombe, kondoo, farasi, twiga, nguruwe, punda, nyati, tembo na wengine wengi. Wanyama kama kuku, bata, nyoka, samaki n.k hawako katika kundi la mamalia kwa sababu hawazai, hivyo hawawezi kupata ugonjwa huu.

**USAMBAAJI/UENEAJI WA KICHAA CHA MBWA**

Ugonjwa wa kichaa cha mbwa unaea kwa njia ya mate kutoka katika mnyama mwenye ugonjwa kwenda kwa mnyama mwingine asiye na ugonjwa. Mate haya yanaweza kumfikia mnyama mwingine kwa njia ya kuuma au kumtemea mate kwenye maeneo yenye vidonda, machoni, puani, mdomoni au mara chache kwa njia ya hewa. Pia vijidudu vya ugonjwa huu vinaweza kusambaa kwa niia ya kunywa maziwa yasiyochemshwa, lakini inasemekana kutoambukizwa kwa njia ya damu, mkojo au kinyesi.

Virusi wa ugonjwa watabaki kwa muda fulani katika eneo waliloingilia kabla hawajaanza kusafiri kupitia mfumo wa fahamu wa pembezoni kwenda mfumo wa fahamu wa kati na kisha huelekea kwenye ubongo (kichwani). Wafikapo kwenye ubongo virusi hawa huanza kuzaliana kwa kasi sana (mgawanyiko wa kirusi kimoja kuwa viwili wakirudia tena na tena na kuwa wengi) na kupelekea kujitokeza kwa dalili kwasababu mfumo wa fahamu unaharibiwa na virusi hao. Kisha kirusi huanza safari nyingine kutoka kwenye ubongo kwenda kwenye matezi ya mate kwa kupitia mfumo wa fahamu wa pembezoni ambapo hutoka pamoja na mate mdomoni.




**Mzungungo wa virusi ndani ya mnyama tangu kuingia hadi vinapotoka**

Muda tangu virusi waingie mwilini hadi dalili kuanza kujitokeza inatofautiana kutegemeana na aina ya kirusi pamoja na umbali kirusi kilipoingilia hadi kwenye ubongo. Hii inafanya kirusimkiweze kusambazwa kwa wanyama wengine hata kabla ya dalili kuanza kuonekana. Muda wa kupata virusi vya ugonjwa hadi kuanza kwa dalili kwa kawaida unaweza kuwa kati ya wiki 3 hadi 12, lakini unaweza kuanzia siku chache hadi miezi kadhaa na mara chache sana kuzidi miezi 6.  Na mara nyingi kwa mbwa huwa kati ya siku 21 hadi 80 tangu apate virusi vya kichaa cha mbwa.

Msambazaji mkuu wa ugonjwa wa kicha cha umbwa ni mbwa (jina la ugonjwa latoka hapa) na wa pili ni paka. Wanyama wengine kama popo pia wanauwezo wa kusambaza ugonjwa huu kwa mwanadamu na kwa wanyama wengine hasa maeneo ambayo usambazi kwa njia ya mbwa na paka imezibitiwa. Wanyama wengi wa porini (kama wanavyoonekana kwenye ramani ya dunia hapa chini) ni watunzaji wakubwa wa virusi vya ugonjwa huu na wanauwezo wa kuusambaza pia kwa wanyama wengine.




Ramani ya dunia kuonyesha aina ya wanyama wanaoeneza kichaa cha mbwa kwa kila nchi

**DALILI ZA KICHAA CHA MBWA**

Dalili za kutegemea bila kujali aina ya mnyama ni mabadiliko ya tabia (kukosa hamu ya kula, kuwa na hofu/wasiwasi, kukasirika haraka, huhamaki/husisimuka, kubadilika sauti, kupoteza hofu kwa watu- mnyama mpole ghafla huwa mkali) na kupooza kusikoelezeka.

**A) Kwa Mbwa**

Dalili za kichaa cha mbwa kwa wanyama zinatofautina kutoka mnyama mmoja na mwingine kutegemeana na madhara yaliyotokea kwa mnyama husika. Dalili halisi za ugonjwa ni pamoja na mabadiliko ya haraka sana ya tabia za mnyama, kupooza kunakoongezeka hatua kwa hatua kunakopelekea kifo cha mnyama. Lakini wanyama wengine wanaweza kufa haraka bila hata ya kuonyesha dalili halisi za ugonjwa. Kwa wanyama dalili hizi zinaweza kugawanywa katika sehemu zifuatazo:

***i-Hatua isiyo onyesha dalili***

-Hapa mnyama anakuwa yupo kati ya siku 10 hadi 90 tangu aumwe na mnyama mwenye ugonjwa na kipindi hiki huchukua siku 1 hadi 3.

-Mnyama anaweza kufa bila ya kuonyesha dalili

***ii- Kughadhibika:*** Virusi kushambulia mfumo wa kati wa fahamu

Hujulikana kama dalili za kichaa cha mbwa japo wanyama wote hupata dalili hizi.

Hapa virusi huanza kushambulia mfumo wa kati (misuli ya fahamu ya mikono na miguu, uti wa mgongo pamoja na ubongo). Hapa ni mara chache kuona dalili za kupooza, na hii hujulikana

-Dalili za mfumo wa upumuaji na chakula hujitokeza (kutoka mate mengi mdomoni, kuhema kwa nguvu, kushindwa kula)

-Mabadiliko ya kitabia na kimhemko hujitokeza (kuwa na hasira kali, kula vitu kama karatasi, kinyesi,fimbo, nyaya na mawe /kushambulia watu na wanyama kwa meno, kucha, pembe na kwato bila hata ya kuwachokoza, kuona vitu visivyoonekana-maruweruwe, hataki kusikia kelele)

-Maumivu na muwasho sehemu iliyoumwa na mnyama hujitokeza (50%)



Wanyama wakiwa na hasira kali sana wanaweza kuuma watu na vitu bila ya kughadhibiwa

***iii-Kupooza na kuanguka:*** Dalili za mfumo wa fahamu

Hapa maambukizi yamesambaa sana kwenye ubongo na virusi wameanza kuharibu ubongo na mnyamahuanza kupooza.

-Kupooza huanza kuonekana kuanzia kwenye koromeo na mashavu huku kukiwa na kutoka mate mengi na machozi na kushindwa kumeza vitu. Mashavu ya chini hulegea na kushuka chini hasa kwa umbwa.

-Mnyama huwa si mkali na hawezi kuuma

-Kuogopa kunywa maji (hydrophobia)

-Kuogopa hewa isimpige usoni (Aerophobia)

-Kuchanganyikiwa na kupata kizunguzungu

-Kupooza kwa mwili kunakoongezeka na hatimaye kupooza kabisa



Dalili za wanyama waliopooza

**iv-*Kuzimia na kufa***

-Mnyama kuwa kwenye usingizi mzito (Kuzimia)

-Mapigo ya moyo huacha kufanya kazi kwa sababu mwili wote umepooza

-Moyo huwa umevimba

-Kwa kawaida mnyama hufa ndani ya siku saba na sababu kuu ni kutofanya kazi kwa mfumo wa damu unaotokana na kupooza kwa mwili wote.



Mnyama aliyekufa kwa kichaa cha mbwa

**B) Kwa mwanadamu**

Wanadamu hupata ugonjwa huu wakiumwa na mbwa mwenye ugonjwa, lakini pia kwa kugusa ubongo na uti wa mgongo wa mnyama mwenye ugonjwa, au kwa kuvuta hewa toka kwenye viungo vya mnyama mwenye ugonjwa. Mara nyingi dalili kwa mwanadamu huanza kujitokeza kuanzia mwezi 1 hadi 3 tangu aumwe na mnyama mwenye ugonjwa. Lakini kumbumbu za tukio moja zinaonyesha kuwa mwanadamu aliwahi kukaa na virusi hadi miaka 7 bila kuonyesha dalili.

Kwa mwanadamu dalili zikisha anza kupona huwa ni majariwa tu na vifo hutokea ndani ya siku 2 hadi 10 tangu kuanza kwa dalili. Kwa bahati nzuri matibabu kabla ya dalili huwa yanafanya kazi vizuri na huokoa uhai.

Dalili zenyewe ni kama zifuatazo:

-Homa, kuumwa kichwa, kuvimba na kuwashwa koo

-Kuwa muoga, kuchanganyikiwa pamoja na kuwa na tabia zisizo za kawaida

-Maumivu/muwasho sehemu iliyoumwa

-Kuona vitu ambavyo havipo (maruweruwe) (Hallucinations) na kufanya ajifiche kwenye kona au akimbie

-Kuogopa maji (hydrophobia) kutokana na matatizo kwenye koo

-Mwili kupooza (kushindwa kuchezesha sehemu/viungo vya mwili) na hushindwa kula chakula

-Mgonjwa hushitushwa na mwanga pamoja na kelele

-Kupoteza fahamu na kufa

**UTAMBUZI WA UGONJWA**

Si rahisi kutambua ugonjwa huu kwa kutumia dalili zilizotajwa hapo juu na hasa kwa maeneo ambayo hautokei mara kwa mara kwani zinafanana na magonjwa mengine. Dalili hizi zitasaidia kuhisi kuwa mnyama (mbwa) anaweza kuwa na ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Na uonapo dalili hizo toa taarifa kwa mtaalamu wa mifugo aliyekaribu nawe huku mbwa akiwa amefungiwa vizuri asije dhuru watu. Utambuzi kamili unafanyika kwenye maabara kwa kupeleka kichwa (ubongo) wa mnyama aliyehisiwa kuwa na ugonjwa.

**JINSI YA KUKABILIANA/KUDHIBITI UGONJWA WA KICHAA CHA UMBWA**

Shirika la afya duniani (WHO) limeweka muongozo unaojitosheleza wa kupambana na huu ugonjwa kama ifuatavyo:

1-Kutoa taarifa ya mnyama (mbwa) anayehisiwa kuwa na ugonjwa wa kichaa cha umbwa na kuangamiza mbwa aliye na dalili za ugonjwa au mbwa aliyeumwa na mnyama mwenye ugonjwa,

2-Kuzuia wanyama katika eneo lililo na mnyama mwenye ugonjwa kwa kuweka karantini ili ugonjwa usisambae,

3-Kunja mbwa wote kwa wakati mmoja na kuendelea kuchanja mbwa wote watakaozaliwa,

4- Kudhibiti mbwa wanaotangatanga (mbwa wasitembee ovyo) na kuangamiza mbwa wote ambao hawajachanjwa

5- Kusajiri mbwa wote

NB: Kwa sababu ya ongezeko la ugonjwa huu kwa paka, paka pia wanapaswa wachanjwe.

-Ni vema raia wakapewa elimu ya kukabiliana na ugonjwa huu kwa ni ugonjwa hatari sana.

***UCHANJAJI***

***Mbwa na Paka:***

Mbwa na paka wanaweza kuanza kuchanja wiki ya 12 au zaidi kwa wale waliochelewa kuanza na kutegemeana na mtaalamu wa eneo husika, kisha baada ya mwaka mmoja.

***Mwanadamu***

Watu pia wanaofanya kazi katika mazingira hatarishi kama madaktari wa mifugo, wanajihusisha na mifugo, walio kwenye maabara zinazochunguza ugonjwa wa kichaa cha mbwa na wale wanaotarajia kusafiri maeneo ambako ugonjwa huu upo wanatakiwa wapewe chanjo. Chanjo yenyewe huchomwa begani kwa mtiririko huu:

Dozi ya 1: Siku ya kwanza

Dozi ya 2: Siku 7 tangu dozi ya 1

Dozi ya 3: Siku 21 au 28 tangu dozi ya 1

Lakini kwa watu wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi wanatakiwa kuangalia mara kwa kinga yao dhidi ya ugonjwa na kuchanja kwa kadri itakavyo hitajika.

**UKIUMWA NA UMBWA UFANYEJE?**

Mbwa au paka akiuma mtu lakini hana dalili yeyote ni vema akawekwa chini ya ungalizi (afungiwe kwenye banda) kwa muda wa siku 10 kama hata onyesha dalili basi anaweza kuwa hana ugonjwa. Na kama ataonyesha dalili basi mbwa auawe na kichwa kipelekwe kwa maabara kwa wataalamu ili uchunguzi zaidi ufanyike.



Mbwa na paka wanaodhaniwa kuwa na ugonjwa wa kichaa cha umbwa wamefungiwa kwa uchunguzi zaidi

Ukiumwa na mnyama yeyote osha kidonda chako haraka vizuri kwa maji safi ya moto na sabuni. Na kama unahisi mbwa/paka aliyekuuma anaweza kuwa na ugonjwa wa kichaa cha umbwa ni vema ukamuona daktari mapema ili aweze kukuanzishia matibabu kwani dalili zikishaanza ni mdogo sana na kifo ni ndani ya siku kati ya 2 hadi 10.

Kwa mtu ambaye ameumwa na mbwa na hakuwahi kuchanjwa dhidi ya ugonjwa huu anatakiwa apewe **dozi 4,** ya kwanza siku hiyo hiyo (inayoambatanishwa na kinga/*immunoglobulins*), kisha dozi nyingine siku ya 3, 7 na ya 14. Kwa mtu aliyewahi kuchanjwa dhidi ya ugonjwa apewe chanjo mbili, moja palepale (kinga kwake si muhimu) na nyingine siku ya 3.